**LEARNING BY EAR - "Girls' Rights"**

**EPISODE 8:**

**Title: Leadership - Mentoring – A Story of Girls' Rights**

**AUTHOR: Njoki Muhoho**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Michael Lawton**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters:**

**SCENE 1 - SCHOOL ASSEMBLY**

Narrator - 30s Male
Cheptoo - 15 Female
Students mixture
Fatuma - 14 Female
Abdi - 15 Male
Headmaster - 40s Male

**SCENE 2 - CIRO PARENT'S HOMESTEAD**

Ciro - 14 Female
Mama Ciro - 40s Female

**SCENE 3 - SCHOOL COMPOUND**

Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Abdi - 15 Male
3 Boys - 14/15s Male

**SCENE 4 - PLAYING FIELDS**

Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Abdi - 15 Male
Fatuma - 14 Female
Narrator - 30s Male

**SCENE 5 - TEACHER MONA'S OFFICE**
Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Fatuma - 14 Female
Teacher Mona - 35 Female
About 4 mixed students (14-16)

**SCENE 6 SCHOOL YARD**
Ciro
Cheptoo
Abdi
Fatuma
Narrator
5-8 mixed students (14-16)

**SCENE 7 - SCHOOL ASSEMBLY**
Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Fatuma - 14 Female
Abdi - 15 Male
Headmaster - 40s Male
Narrator - 30s Male
5-8 mixed students

**01. <u>INTRO</u>**

**02. <u>MUSIC: THEME MUSIC</u>**

03. **NARRATOR** Hujambo na karibu kwa makala ya nane ya mfululizo wa vipindi vya 'Learning By Ear' Noa Bongo Jenga Maisha yako katika mchezo huu kuhusu **Haki za Wasichana**.Katika kipindi kilichotangulia Fatuma, Ciro na Cheptoo wamerudi shuleni baada ya kufukuzwa kwa muda wa wiki mbili. Fatuma, Ciro, Cheptoo wamejikuta mashakani kutokana na ushawishi wa kuiga tabia mbovu miongoni mwa vijana wa rika lao.
Katika kipindi cha leo tunageukia suala la Haki za wasichana kuhusu Uongozi. Tuungane na wasichana hawa wanapojadilia hoja hii katika bunge lao la waischana.

**<u>SCENE 1: SCHOOL ASSEMBLY</u>**

**04. <u>SFX: STUDENTS MURMURING (studio)</u>**

05. **HEADMASTER** Hamjambo wanafunzi.

06. **STUDENTS** Hutujambo Mwalimu mkuu.

| | | |
|---|---|---|
| 07. | **HEADMASTER** | Kama mnavyofahamu, hivi karibuni tutakuwa tukiandaa uchaguzi kuwateua viranja na viongozi wa vilabu mbali mbali shuleni. Wale wote wanaotaka kugombea nyadhifa hizi wanapasa kuwasilisha majina yao kwa Mwalimu Mona ambaye atakuwa msimamizi wa uchaguzi huu.Kuwambukusha tu ni kwamba,uchaguzi huu ni kutafuta uongozi bora. Kuwawachagua watu wenye tajriba ya Uongozi. Wagombeaji lazima wawe watu wenye sifa nzuri,wa kujiamini na kujitolea. Wote wanaotaka kugombea nyadhifa hizi lazima wahakikishe wanatimiza masharti haya kabla ya kuwasilisha majina.! |
| 08. | **CHEPTOO** | (LOUD WHISPER) Unafaa kabisa kugombea wadhifa katika uchaguzi huu. |
| 09. | **FATUMA** | Cheptoo, ni kawaida yako kujitakia makuu na sifa. |
| 10. | **ABDI** | (LOUD WHISPER) Nyamazeni hapo nyinyi wasichana. Hii ndio sababu hamuwezi kuwa viongozi. |
| 11. | **HEADMASTER** | (LOUDLY) Nyamazeni hapo! |

**12. <u>BRIDGE MUSIC</u>**

**<u>SCENE 2 CIRO PARENT’S HOMESTEAD</u>**

**13. <u>SFX: FARM NOISES</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 14. | **CIRO** | Mama, Rafiki yangu Cheptoo anataka kugombea wadhifa wa kiranja mkuu wa kike Shuleni. Miaka yote tumekuwa tu na viranja wa kiume. Unadhani huu ni uamuzi wa busara!.Yeye ni rafiki yangu na nina wasi wasi sana. |
| 15. | **MAMA CIRO** | Tayari nyinyi wasichana mnaandamwa na matatizo chungu nzima shuleni kando na masuala ya uongozi………. |
| 16. | **CIRO** | Kwani msichanaa hawezi kuwa kiranja? |
| 17. | **MAMA CIRO** | Mwache rafiki yako Cheptoo aendelee na wazimu wake!. Yeye ni kimbelembele sana... Kwani hujui…? Lakini mwache ajaribu bahati yake!. Navyojua haitakuwa rahisi hivyo anavyofikiria. Atakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa hao wavulana wakati huu.Kwamba yeye ni msichana na hawezi kuongoza.Lakini ni bora kujaribu ndio awe mfano kwa wengine. |

**18. BRIDGE MUSIC**

**SCENE 3  SCHOOL COMPOUND**

19. **SFX: SCHOOL YARD NOISES**

| | | |
|---|---|---|
| 20. | **CHEPTOO** | Wanafunzi ..wanafunzi wenzangu, ,…. Wakati sasa umewadia kwa shule hii kumteua kiranja mkuu wa kike.. Na mimi niko tayari. |
| 21. | **BOYS** | BOOOOOO OOOOOO |
| 22. | **ABDI** | (mimicking) Eti  wakati umefika ….wakati wa gani? Cheptoo, wasichana hawawezi kuongoza…!Umechemsha Cheptoo shuka jukwaani! Tayari nimefanya kampeini ya kutosha kote shuleni humu kutaka ni nichaguliwa kama kiranja wa shule. |
| 23. | **CIRO** | Abdi,wewe ni binamu yangu… lakini unajidanganya…! nini kinachokufanya ufikirie kwamba Cheptoo hawezi kuwa kiranja Mzuri kuliko wewe? Mupe nafasi ya kufanya kampeini zake. |

| | | |
|---|---|---|
| 24. | **ABDI** | Nyenye nyenye,…. Haya mwache Cheptoo afanye Kampeni… anapoteza muda wake tu.Kwani umenisikia mimi nikumuuliza anipe nafasi ya kufanya kampeini? Kwani yeye ndio maalum sana. Anapoteza bure pumzi zake. |
| 25. | **CHEPTOO** | Nisikilizeni,….. nisikilizeni nyinyi wavulana na wasichana. Abdi…,mimi sikuomba nafasi ya kufanya kampeni, mimi ni kama wewe tu, kutangaza nia yangu ya kutaka kungombea wadhifa huo wa Kiranja mkuu shuleni.Wewe fanya kampeni zako, na mimi nitafanya kampeni zangu. Lazima ufahamu kwamba wasichana pia wanaweza kuwa viongozi bora! |
| 26. | **ABDI** | (SHOUTING) Wacha kujisumbua,wasichana ni watu kama bendera tu kufuata upepo na wala hawawezi kuwa viongozi. Kazi yenu ni wake nyumbani na si vinginevyo. |
| 27. | **CIRO** | Cheptoo.. Chepii.. Chepiii.. punguza hasira... Tuyaache haya kwa sasa..twende tukalijadilie suala hili. |
| 28. | **CHEPTOO** | Sawa.. Ciro.. Nisaidie kushuka. |

| | | |
|---|---|---|
| 29. | **CIRO** | Sawa Madam Kiranja mkuu. (HEAVES) Na … Na wewe Abdi, kusanya wavulana wenzako twende kule uwanjani, kujadilia suala hili la uongozi. |
| 30. | **ABDI** | Sawa!! Tunakuja kuwasikiza mna lipi la kutwambia nyinyi wasichana. |

**31. <u>BRIDGE MUSIC</u>**

**<u>SCENE 4 PLAYING FIELDS</u>**

**32. <u>SOUNDS: PLAYING FIELDS SOUNDS</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 33. | **CIRO** | Nawasilisha hoja kwamba wasichana wanauwezo kama wanaume au pengine hata zaidi ya wanaume kwa masuala ya uongozi katika jamii. |
| 34. | **ABDI** | Nimesema mara kwa mara, wasichana hawawezi kuongoza, ni wadhaifu mno!. |
| 35. | **CHEPTOO** | Unaweza kusema hivyo mbele ya mwanamazingira mashuhuri Profesa Wangari Mathaai au Rais wa Liberia Ellen Johnson Sirleaf? Yaani kuna Wanawake ambao wameonesha vipawa vya uongozi duniani, bila ya kumsahau Kansela wa Ujerumani Angela Merkel. |

| | | |
|---|---|---|
| 36. | **ABDI** | Ni kweli ….ni kweli …lakini ni wachache sana |
| 37. | **FATUMA** | Pia kuna wanawake ambao ni machifu, Mawaziri…na kadhalika! |
| 38. | **ABDI** | Hatukatai kwamba wako. Lakini ni wangapi?Hii ni kumaanisha si wengi wanaoweza!. |
| 39. | **CIRO** | Abdi, Unaniudhi sana. Hebu niambie, ni nini wavulana wanaweza kufanya ambacho wasichana hawawezi. |
| 40. | **ABDI** | aaaggggh.. Nyinyi ni wadhaifu tu.Nichagueni mimi kama kiranja.. Mpigieni kura kuongozi shupavu! |
| 41. | **CHEPTOO** | Unasema nini? Eti sisini wadhaifu.. wadhaifu…ukubali tu kwamba unatuogopa. |
| 42. | **ABDI** | Kuogopa? kuogopa? Kukuogopa wewe? |
| **43.** | **<u>SFX: BELL RINGS</u>** | |
| 44. | **CIRO** | Sasa waona ulivyofanya?. Hata hatujaanza kujadili hoja hii. |

45. **CHEPTOO** Upesi turudi darasani. Kisha baadaye tutamuliza Mwalimu Mona kuungana nasi kwa mjadala huu mkali.

**46. BRIDGE MUSIC**

47. **NARRATOR** Na kweli haikuwachukua muda.Mjadala ukarejea bungeni Tuungane nao kusikiliza hoja zao wanapokutana na Mwalimu Mona.

**SCENE 5 TEACHER MONA'S OFFICE**

**48. SFX: office, people quietly talking in the background**

49. **CHEPTOO** Mwalimu Mona, tusaidie tafadhali.

50. **TEACHER MONA** Ni msaidie vipi wasichana?

51. **CIRO** Cheptoo anafanya kampeini za kutaka kuchaguliwa kama kiranja mkuu wa shule, lakini wavulana wanamdhihaki.

52. **CHEPTOO** Pia Ciro anataka kuwa kiranja wa darasa letu lakini anaogopa kubezwa na au kuudhiwa.

53. **TEACHER MONA** Ooh maskini.

54. **CHEPTOO** Sasa tufanyaje. Watu wanasema ni sisi tunafanya mzaha tu, na Fatuma hapa ame… ame..

| | | |
|---|---|---|
| 55. | **FATUMA** | Nimeogopa Mwalimu. Nina wasi wasi kuhusu marafiki zangu.Nawaomba wafutilie mbali wazo la kugombea nyadhifa hizo wakati wa uchaguzi ujao. |
| 56. | **TEACHER MONA** | Fatuma.. Fatuma.. Hayo ndio maombi na matakwa ya waulana Wanataka mjiondoe kwenye kinyang;anyiro hiki ili wasalia wao pekee, na kupata ushindi wa bwerere. Mutakubali? |
| 57. | **FATUMA** | Hapana Mwalimu. |
| 58. | **TEACHER MONA** | Nafurahi sana kusikia hilo. |
| 59. | **CHEPTOO** | Nina wazo. Pengine tupange njama za kuiba kura! |
| 60. | **ALL** | Cheptoooooo!!! |
| 61. | **CHEPTOO** | Nilikuwa natania tu. |
| 62. | **TEACHER MONA** | Kwanza nyinyi wasichana kuna mengi sana ya kujifunza kuhusu suala la uongozi. Pili, mnahitaji kupanga mikakata ya kutangaza sera zenu. Na kuna masuala mengi sana ya kuzungumzia kuhusu uongozi … Haya yote ni mambo mnayohitajika kufanya.. |

**63. <u>BRIDGE MUSIC</u>**

**64. SCENE 6 SCHOOL YARD**

65. **NARRATOR** Mwalimu Mona amechukua jukumu la kuwaongoza na kuwaelimisha wasichana kuhusu masuala ya uongozi. Hebu tusikie yatakayojiri.

**66. SFX: School yard**

67. **CIRO** Tunahitaji kiongozi ambaye anaelewa mahitaji yetu. Kiongozi ambaye atatekeleza na kutimiza ahadi.Kiongozi ambaye atakuwa kielelezo na mwenye maono. Kiongozi, ambaye anaweza kutoa ushauri na mwelekeo wakati mambo yanapokwenda kombo na si mwenye kulegalega.Huyo ndie kiongozi tunayemtaka.Sasa tumkaribishe mgombeaji wetu Cheptoooo!.

**68. SFX: GIRLS CLAPPING AND CHEERING; BOYS BOOING (studio)**

| | | |
|---|---|---|
| 69. | **CHEPTOO** | Nimesimama hapa mbele yenu kama kiongozi wenu mtarajiwa. Suala ibuka hapa si iwapo tunamchagua kiongozi msichana au Mvulana. Msingi ni kumpata kiongozi shupavu, mwenye uwezo wa kutuongoza na kutuleta pamoja. |
| 70. | **ABDI** | Vipi utaweza kusimama mbele ya wanaume na wakusikize? Watakusikiza kweli?. Afadhali mimi wanaweza kunisikiliza, wao ni wanaume kama mimi lakini sio wewe! |
| 71. | **CHEPTOO** | Mimi nazungumzia sera na uongozi bora.Masuala yanayotukabili sisi sote iwe msichana au mvulana.Usafi shuleni, uhusiano mwema baina ya wanafunzi na waalimu, Kudumisha nidhamu na kadhalika.Nitamwakilisha na kuwasilisha vyma maoni yenu kwa wasimamizi wa shule. |
| 72. | **ABDI** | Unayozungumza ni ya maana sana. Na nmejfunza mengi kutoka kwako! Si mzaha! |

| | | |
|---|---|---|
| 73. | **CHEPTOO** | Kama kiongozi, maneno ninayozungumza huwa ni ya maana sana na yenye manufaa kwa wote.Hapa hatuzungumzii tofauti za kijinsia.Abdi, unazungumza kwa niaba ya wavulana pekee katika sera zako? Ni vipi wasichana wataweza kukuchagua kwa kuzingatioa na mbinu hizo za uongozi? |
| 74. | **ABDI** | Sawa..sawa.. sawa. Nilikuwa nikitaka kusema hivi….unajua.,, |
| 75. | **CIRO** | Kura kwa  Cheptoo, Kura kwa Cheptoo.. Kura kwa Cheptoo, |
| 76. | **FATUMA** | Mpigieni kura Cheptoo kama kiranja mkuu. |
| 77. | **ABDI** | (LOUD WHISPER) Ehhh.. Nimeanza kushawishika au vipi?  Sawa tutaona nani atakaye ibuka mshindi wakati wa uchaguzi. Wapiga kura ndio waamuzi sio mimi au wewe! |
| 78. | **CIRO** | Abdi, Nimekusikia viruzi au ni masikio yangu? |

| | | |
|---|---|---|
| 79. | **ABDI** | Ndio .. Sasa nimeshawishika kwamba Msichana pia anaweza kuongoza. Baadhi yetu tumekuwa tukipayuka tu na kuchukulia vivi hivi eti wasichana hawawezi kuongoza kwasababu ya jinsia yao.Kumbe tunajidanganya!. Hata hivyo lakini tusubiri uchaguzi. |
| 80. | **FATUMA** | Mimi nashangaa mawazo hayo yote unayatoa wapi?. Lazima ni kutokana na ushauri tunaopewa!. |
| 81. | **CIRO** | Ndio… sisi wasichana tumekuwa tukiamini kwamba hatuwezi kuongoza. Lazima sasa tujiamini.Wavulana wanajidanganya kwamba ni wajibu wao kuwatunza wasichana na pia kushikilia yadhifa za uongozini siku zote.Mambo hayo yamepitwa na wakati na sasa kasumba hiil lazima ibadilike…! mambo yamebadilika sasa….! |
| 82. | **CHEPTOO** | Sasa tumepata ufahamu zaidi. Najiamini kwamba naweza kufanya kampeini na kuwashawishi watu kuzingatia uwezo wangu na wala sio kubaguliwa kwa misingi ya jinsia. Kura kwangu, mpigie kura Cheptoo! |

**83. <u>BRIDGE MUSIC</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 84. | **NARRATOR** | Ama kwa hakika Cheptoo amefaulu kubadili mtazamo wa wavulana kwa wasichana, lakini je atafaulu kuchaguliwa.? |

**<u>SCENE 7: SCHOOL ASSEMBLY</u>**

**85. SFX: students' noise (studio)**

| | | |
|---|---|---|
| 86. | **HEADMASTER** | Wanafunzi, kama Mwalimu wenu mkuu, nachukua fursa hii kutoa pongezi kwenu nyote kwa jinsi mlivyoendesha uchaguzi uliopita. Leo tumeweka Historia na sasa ningependa kutangaza matokeo.<br><br>(CLEARS THROAT)<br><br>Kiranja wetu mkuu ambaye ataaza kuhudumu tekeleza jukumu lake kuanzia mwaka ujao niiiiii…….. Cheptoooo…!!! |

**87. SFX: STUDENTS CHEERING AND CLAPPING**

| | | |
|---|---|---|
| 88. | **CHEPTOO** | Tumefaulu… tumefaulu, sasa tumefaulu |
| 89. | **CIRO** | Cheptoo…Umenifurahisha sana.Kwa kweli wewe ni farahari yangu. |
| 90. | **FATUMA** | Cheptoo…..Umeshinda, umeshinda… |

| | | |
|---|---|---|
| 91. | **CHEPTOO** | Si kwa juhudi zangu pekee bali pia ni juhudi zenu ndiposa tumefaulu. Mmetekeleza jukumu kubwa na muhimu sana wakati wa Kampeini. Na huu si ushindi wangu peke yangu,ni wetu sote, Wavulana kwa wasichana!. Namshukuru nyote.Na zaidi ningepeza ushirikiano wenu wakati ninapoanza kutekeleza jukumu langu kama kiranja mkuu. |
| 92. | **CIRO** | Kweli…. Kweli kabisa…. sasa unazungumza kama kiongozi. |
| 93. | **ABDI** | Hasaa, umezungumza kama kiongozi tumtakaye. Pongezi sana kiranja wetu. |

**94. <u>THEME MUSIC</u>**

**95. OUTRO**

96. **NARRATOR**

Imekuwa ni safari ndefu yenye mabonde na milima katika kutafuta uongozi. Na sasa wasichana hawa wamefaulu katika jitihada zao. Cheptoo ni sharti aonyeshe uwezo wake wa kuongoza! Ungana nasi tena kwa makala ijayo usikie jinsi wasichana watakavyokuwa wakijadilia suala la ngono.Na iwapo ungependa kusikiliza tena kipindi hiki au vingine , tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwa makala nyingine kwaheri kwa sasa.